

raini yenye mramani ya Sh 500,000  
walipeleka malalamiko kwa viongozi  
wao wakitaka kufahamu iwapo fedha

Alipohojija sababu ya ofisi  
yake kutokuwa na choo, amesema:

zikiambatana na dunia hii  
ni risiti halali ya serikali.

JAMHURI UK 16.

# \* Mifugo, uvuvi watakiwa kushiriki AGRF 2023

DODOMA

NA MWANDISHI WETU

Waziri wa Mifugo na Uvvi, Abdallah Ulega,  
amewataka wadau wa sekta za kilimo na uvuvi nchini  
kujisajili kushiriki Mkutano wa Jukwaa la Mifumo ya  
Chakula Afrika (AGR 2023).

Mkutano huo mkubwa barani Afrika unatarajiwa  
kufanyika nchini Septemba mwaka huu.

Akizungumza jijini hapa mwishoni mwa wiki,  
Ulega, amesema hiyo ni fursa kwa wadau kuzitangaza  
biashara na kupata mitaji na masoko.

"Wizara imeshakutana na wadau zaidi ya 300  
kama sehemu ya kuwaandaa, kuwahamasisha  
kujiandikisha na kushiriki mkutano huo unaolenga  
kufungua milango ya uwekezaji na kuongeza  
uashirikiano kibiashara," amesema.

Amesema dhima ya mkutano wa AGRF 2023 ni  
kuwawezesha vijana na wanawake kushiriki kikamilifu  
katika mnyororo wa thamani wa mfumo wa chakula.  
Rais Dk. Samia Suluhu Hassan ameshaanza  
kutekeleza azima hiyo kwa vitendo.

Waziri amewataka wadau kuvisajiri kupitia tovuti  
ya AGRF: [www.agrf-inperson.com](http://www.agrf-inperson.com), ambapo timu ya  
wataalamu wa wizara kwa kushirikiana na kamati  
ya maandalizi kitaifa warnejipanga kutoa msaada wa  
kitalaamu.

"Nampungeza Rais Samia kwa hatua mbalimbali  
anazozichukua kuwaletea Watanzania maendeleo,  
mfano programu inayoitwa 'Building Better  
Tomorrow for Livestock and Fisheries Entrepreneurs',  
ambapo vijana 738 kwa awamu ya kwanza kati ya hao



Waziri wa Mifugo na Uvvi, Abdallah Ulega.

238 kutoka sekta ya mifugo na wengine 500 kutoka  
sekta ya uvuvi wamekwisha kunufaika," amesema  
Ulega.

Mbali ya kunufaika na mitaji, vijana hao walipewa  
mäfunzo ya unenepeshaji mifugo, majongoo bahari  
na ufugaji wa samaki kibiashara sambamba na  
kupewa mitaji kwa ajili ya ununuzi wa ng'ombe  
na kuwezesha miundombinu na upatikanaji wa  
masoko ya uhakika. Waziri amesema AGRF 2023 ni  
nafasi adhimu kwa Tanzania kuiweka ramani yake  
kwa dunia na Afrika kwa ujumla wake kuwa ipo  
katika nafasi nzuri ya kuzalisha bidhaa mbalimbali  
zinazotokana na mifugo na uvuvi.

Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Utafiti wa  
Mifugo (ILRI), Profesa Appolinaire Djikeng,  
amesema wawekezaji wanataka kuhakikishiwa  
uhakika na usalama katika uwekezaji ambao  
wanaufanya.

"Tanzania ina mazingira mazuri ya uwekezaji na  
ndicho kitu ambacho wawekezaji wangependa kuona  
maeneo mengi barani Afrika. Tupo tayari kufanya  
kazi na vyombo vya habari kuitangaza AGRF,"  
amesema Profesa Djikeng.

# 'Tanzania can feed the rest of Africa'

By Polycarp Machira, Dodoma

TANZANIA is ready to feed the rest of Africa with first class protein as it hosts the Africa's Food Systems Forum, Minister for Livestock and Fisheries, Abdallah Ulega has said.

Speaking while calling on players in livestock and fishery sectors to register and come in large numbers to the international meeting scheduled for September in Dar es Salaam, he said livestock and fisheries have a big stake in the forum.

He said the forum provides an opportunity for locals to partner with international investors, adding: "We want people to invest in Tanzania and the time has now and these sectors have great significance as the forum is expected to bring together 3,000 stakeholders in food systems and value."

Speaking here over the weekend on how his ministry has prepared to ensure that its stakeholders

register for the summit, he said the summit among others would promote opportunities existing in the sectors.

He said those stakeholders wanting to register should visit the ministry's website and find AGRF website [www.agrf-inperson.com](http://www.agrf-inperson.com) where experts from ministry work with AGRF national preparation committee to ensure everything goes as planned.

The minister said this year's AGRF 2023 is committed to empowering youths and women to participate in food systems and value chain.

"Tanzania has made significant strides in promoting food security, sustainable agriculture and the Africa food systems summit will serve as a platform for the country to share its best practices and forge new partnerships," he explained.

He also applauded President Samia Suluhu Hassan on the recently launched youth agricultural programme dubbed 'Building Better Tomorrow for Livestock and

Fisheries Entrepreneurs' in which 738 youths in livestock and fishery sectors benefit from phase one of the project.

According to him, among the beneficiaries 238 were drawn from livestock while 500 from fishery sector where they were trained and imparted skills and knowledge before, they were given capital and exposed to markets.

The minister said meat and fish fillets exports from Tanzania have increased steadily from 1,774.20 tonnes in 2020/21 to 12,243.79 tonnes in 2022/23 bringing in 51,894,622.44 US Dollars which showed major transformation in the sector.

Tanzania will be the first country to host the AGRF Summit organised by Alliance for a Green Revolution in Africa (AGRA) since rebranded to Africa's Food Systems Forum this year to promote the ambition of transformation of Africa's food system and engagement.


The historic summit among

others will attract over 3,000 delegates among them will include top leaders, thinkers, stakeholders in food systems and value chain and implementers in African food agriculture.

Earlier, the Director General of International Livestock Research Institute (ILRT) Prof Appolinaire Djikeng said investors want assurance and security of their investments wherever they go and invest.

"Tanzania has a conducive environment for investments and this is what investors want to see when they invest in any part of Africa. We are ready to work with the media to promote AGRF," Prof Djikeng said.

ILRI has worked in Tanzania since 1994 on issues ranging from market mechanisms to food safety and livestock policy. In Tanzania, it focuses on sustainable identification of mixed crop-livestock systems through increasing productivity and value chain development.



HABARI LEO UK 12.

# Mkakati wa 3 wa AGRA kubadili kilimo kwa kuhakikisha masoko

Na Mwandishi Wetu

**U**CHUMI wa Tanzania kwa miongo miwili umekuwa ukukua. Kwa kipindi hicho umeendeeka kuwa imara na utekelezaji wa awamu ya pili wa mpango wa maendeleo wa miaka mitano (FYDP II) unaonesha kuwa uchumi unakua kwa wastani wa asilimia 6.9 katika kipindi chote kuanzia 2016/2017 hadi 2020/2021.

Kukua kwa uchumi katika kiwango hicho ni matokeo ya uwapo wa baraka za maliyasi pamoa na taifa kuwa katika eneo bora kijigania linalowezeshu kufanya biashara za usafirishaji kwa nchi zipatazo nane zinazoingunguza.

Pamoja na madini na asilimali nyiningine maridhawa, Tanzania imbarikiwa kuwa na ardhi kubwa yenye uwezo wa kuzalisha bidhaa mbalimbaji kwa kilimo kuanzia chakula hadi malighafi ikiwamo miifugo.

Katika hali halisi na kitakwimu uchumi wa Tanzania unategemea sana kilimo ambacho huchangia asilimia 27 ya Pato la Taifa ikiingiza asilimia 25 ya fedha za kigeni. Sekta hii pia inachangia asilimia 65 ya ajira yote nchini na asilimia 65 ya malighafi inayotumika katika viwanda.

Pamoja na hayo wakulima wadogo ambaa ni wazalishaji wakubwa ndio wanafanya asilimia 70 ya wakulima wanaowezeshu miifumo ya chakula na kilimo nchini. Katika kundi hilo la wakulima wadogo wanawake wanaofanya kilimo ni asilimia 69.

Ingawa nchi imekuwa ikipiga hatua za maendeleo katika kuimarisha sekta, taifa bado halijafikia ukujai wa kilimo wa asilimia 6 unaotakiwa kama iliyoyelezwa katika mpango wa pili wa maendeleo wa miaka mitano na pia Mpango wa Maendeleo wa Kilimo wa Afrika (CAADP) na asilimia 10 ambayo imelengwa na Agenda 10-30, lengo likiwa ni kufikia asilimia 10 ikiapao mwaka 2030.

Pamoja na takwimu hizo, shirika linalojishughulisha na ukujai endelevu wa Mifumo ya Chakula Afrika (AGRA) ambalo limekuwa likifanyakazi na Serikali ya Tanzania tangu 2006, wiki iliyopita lilizindua Mpango Mkakati wa tatu wa AGRA wenye lengo la kuchochaea

masoko jumuishi na yenye ushindani katika kilimo kuleta mabadiliko kwenye miifumo ya chakula nchini na kufanya iwe endelevu.

Katika uzinduzi huo uliosfanywa na Waziri wa Mifugo na Uvuu, Abdallah Ulega, wakiwa na Waziri Mkuu mstaafu, Mizengo Pinda ambaye pia ni Mwenyelekiti wa Baraza la Rais la Chakula na Kilimo, ilielezwa kuwa mkakati huo umelenga kuwajengea uwezo vijina na wanawake wa Kitanzeria katika mnyororo wa thamani wa kilimo na hiyo kukusa ajira, ukujui wa uslasi wa jamii na uchumi.

"Kuna mambo manne katika mkakati huo," anasema Mencia wa AGRA wa Tanzania, Vianey Rweyendela akieleza yatanufaisha zaidi ya wakulima milioni tatu nchini kwa kuwatapatio masoko ya mazao yao.

"Mkakati huo unajumuisha uboreshaji wa upatikanaji wa fedha na masoko na kukuza utumaji wa teknolojia mahiri za hali ya hewa na matumizi ya pembejeo, kama vile mbegu na mbolea," anasema Rweyendela.

Ukiusoma mkakati huo unaona umelenga kuwa na jukwaa thabitibni la kushirikisha maarifa na ubunifu na kukuza mijadala yenye maarifa kuhusu changamoto katika kilimo na biashara na kuboresha ufikiaji wa afua muhimu za kifedha kwa lengo la kuwezesha matumizi makubwa ya teknolojia na sayansi katika kilimo.

Akizingumzua wakati wa hafla ya kuzindua mkakati huo, Mkuu wa Kikanda wa AGRA Afrika Mashariki, Profesa Jean Jacques Muhinda anasema taasisi yake katika miaka hiyo mitano imelenga kuunga mkono juhudii za Serikali ya Tanzania kuwa na uzalishaji mkubwa wa chakula.

"Tanzania imeonesha umahiri katika kubadilisha miifumo yake ya kilimo cha chakula. Katika kipindi cha miaka mitano ijayo, tunuanu kusaidia kufungua fursa zaidi za kilimo na masoko wakati nchi inapoendelea kufanya mabadiliko chanya kwenye kilimo."

AGRA inafanya kazi na serikali na mashirika binafsi katika kuvutia uwikezezaji, kusaidia magenzi yu sera na kutoza zana za kilimo, maarifa na msada kwa wakulima.

Aidha, AGRA imeshirikiana na sekta binafsi kupitia Tanzania Agro-Industrialization

Development Flagship, TAIDE, (mradhi mkubwa wa kuwezesha maendeleo ya viwanda vya kilimo) kuhamiasisha na kuratibu ubia katika sekta ya umma na sekta binafsi; katika mradhi huo ufadili wa Dola za Marekani milioni 300 zilipatikana na kunufaisha wakulima zaidi ya milioni moja.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Gerald Mweli aktizungumza katika uzinduzi anasema Tanzania imelenga kuwa ghala la chakula kwa nchi za Afrika na duniani kote na hiyo haina budi kufungua uwezo wa sekta ya kilimo na kushukuru AGRA kwa kushirikiana na serikali kufanikisha azma hiyo kwa manufaa ya wakulima wadogo na ya taifa.

Kwa mujibu wa tovuti ya AGRA, shirika hilo ambalo linafanya kazi zake kuwiana na Mpango wa Kuendeleza Sekta ya Kilimo nchini Awamu ya Pili (ASDP II), unaolenga kubadilisha miifumo ya kilimo nchini sambamba na kuongeza tija na kipato kwa wakulima wadogo, baada ya kujenja misingi thabiti ya teknolojia, ubia na miundo, iko tayari sasa kuongeza kilimo chenyet ujumuishi na ushindani nchini kwa kuyafungua masoko.

Mkakati wake wa pili uliotekelizwa 2017-2021 ulilenga kuchochaea na kudumisha mabadiliko ya kilimo jumuishi. Mabadiliko hayo yalilenga kuongeza mapato na kuboresha usalama wa chakula kwa kaya za wakulima wadogo milioni 1.5 kwa kuwekeza Dola za Marekani milioni 28. Kiasi hicho cha fedha kimewekezwa ambapo Dola milioni 11.3 zilisambazwa kupitia ruzuki 31 tofauti ambapo wakulima 742,865 walinufauka.

Aidha, ASDP II umenufaika na ruzuku kubwa ya Dola milioni 1,672. Zaidi ya wakulima 42,000 wamefaidika moja kwa moja na mpango huo, wakiongezeza na wakulima 34,000 walifikiwa kupitia mpango mingire.

Wakati AGRA ikizindua mpango mkakati wake huo mpya, takwimu zinaponesha mauzo ya mazao chini ya mpango ya AGRA yaliutu Dola milioni 1.6 na kuwaweka wakulima katika hali bora zaidi kuliko mpango uliotangulia kwani kwa kiasi kikubwa mkakati wa pili uliletu mabadiliko na ukujai wa sekta ya kilimo nchini.



Waziri Mkuu Mstaafu, Mizengo Pinda (wa tatu kulia) pamoja na Waziri wa Mifugo na Uvuu, Abdallah Ulega wakizundua mkakati wa miaka mitano wa AGRA katika ukumbi wa PSSSF, Dodoma hivyo karibuni. Wengine ni watendaji na wafadhilli wa AGRA.

Na Si

K  
waba  
maen  
Ha  
kwa r  
mashi  
guaji i  
cha sa  
Kj  
Wilay  
maari  
nduri  
ukw  
jikita l  
hilo k  
ghafi.  
T  
turnia  
hadi l  
masu  
kurun  
tunab  
kujip  
Juma  
ubang

Ar  
maga  
mkali  
yote t  
kwa v  
koros  
kubar  
L  
gua u  
3,200  
bure s  
kilo tr  
sha m  
M  
yearn  
moto  
kikwi  
itubo  
chur  
moja  
H  
kijij  
kilo k  
ya Sh  
mazi  
hupa  
hivyo  
C  
wa v  
Haln  
Nam  
tekn  
kwa  
chan  
sekt  
A  
wan  
kwo  
kaw  
kul  
ya i  
vik  
ene

far  
kip  
w  
ji  
w  
v  
n  
v  
d  
!